# Zawadi kwa Nadwa

na

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi[as]

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya
Tanzania

ZAWADI KWA NADWA
Tafsiri ya Kiswahili ya: *Tuḥfatun-Nadwah* (Urdu)

Kilichoandikwa na:
Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian
Masihi Mau'udi na Imam Mahdi[as]
(Swahili translation of *Tuḥfatun-Nadwah*)

Mfasiri: Sheikh Bakri Abedi Kaluta

Chapa ya Kwanza (Kiurdu): 1902
Chapa ya Kwanza (Kiswahili): 2015

© Islam International Publications Ltd.

Kimeenezwa na:
Islam International publications Ltd.
'Islamabad' Sheephatch Lane,
Tilford, Surrey GU10 2AQ, United Kingdom

Kwa maelezo zaidi:
**Tanzania:**
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dare es Salam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744
**Kenya:**
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi, Kenya. Simu: +255222111031

ISBN: 978-1-84880-540-8

# Faharisi

*Maelezo ya mwenezi* ______ *i*

KUHUSU MWANDISHI ______ i

KUHUSU KITABU ______ ii

SHUKURANI ______ iii

*Tabligh* ______ *1*

*Shairi la Mir Nasir Nawab wa Delhi* ______ *5*

*Kijitabu kiitwacho Zawadi kwa Nadwa* ______ *9*

*Bishara kubwa k wa Waislamu wote na kwa ajili ya wote watafutao ukweli* ______ *31*

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ

# Maelezo ya mwenezi

## KUHUSU MWANDISHI

Mwandishi wa kitabu hiki Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa na Imam Mahdi[as] alizaliwa tarehe 13 Februari 1835 huko Qadian, India. Alijitolea maisha yake yote kujifunza elimu ya Kurani Tukufu na kumwabudu Mwenyezi Mungu. Kwa kuona hali duni ya Waislamu na kushambuliwa sana na wapinzani, alimwomba Mwenyezi Mungu kwa unyenyekevu sana kwa ajili ya mafanikio ya Islam. Vile vile alikubali kujibu shutuma za wapinzani na kutetea dini ya kweli. Mwenyezi Mungu Alimchagua kuwa Imamu wa zama hizi. Hivyo aliielezea dunia mafundisho sahihi ya Islam. Kwa kupata lengo hili aliandika vitabu zaidi ya 80 katika lugha ya Kiurdu na Kiarabu. Kwa njia ya kutoa hotuba na kufanya mijadala na viongozi wa dini zingine alifanya kazi ya muhimu ya kueneza na kutetea Kitabu cha Mungu. Alithibitisha kwamba Islam pekee ndiyo dini illiyo sahihi na hai siku hizi inayoweza kujenga na kuimarisha uhusiano kati ya mtu na Mwumba wake. Alitangaza kwamba Mwenyezi Mungu Amemchagua kuwa Imam

Mahdi na Masihi Aliyeahidiwa, sawa na bishara za Biblia, Kurani na Hadithi za Mtume saw. Sawa na amri ya Mwenyezi Mungu alianzisha Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah tarehe 23 Machi 1889 huko Ludhiana, India. Sasa Jumuiya yake inapatikana katika nchi 206 za dunia. Baada ya yeye kufariki, Mwenyezi Mungu Alianzisha nidhamu ya Ukhalifa katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah kuendeleza shughuli zake. Siku hizi Khalifa na Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyyah ndiye Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba].

KUHUSU KITABU

*Tuhfatun Nadwa*, kitabu cha Seyyidna Ahmad[as] kilichapishwa mnamo mwaka wa 1902. Mwanzoni mwa kitabu amewasihi watu wa *Darun Nadwa* kuikubali Kurani Tukufu kuwa mwamuzi, na akadai kuwa Masihi Aliyeahidiwa.

Aliandika katika kijitabu hiki madai yake ya kuwa Masihi Aliyeahidiwa na hoja za ukweli wake kwa ajili ya kusomewa katika mkutano wa *Nadwatul ulamaa* uliopangwa kufanyika katika tarehe 9 hadi 11 Oktoba 1902 huko Amritsar. Vile vile ameeleza kwamba hii si sahihi kabisa kwamba mdai mwongo wa unabii anaweza kuishi miaka 23 baada ya madai yake sawa na muda aliopata Mtume Muhammad[saw] baada ya madai yake.

Hafidh Muhammad Yusuf aliyemkaribisha mkutanoni kusoma makala hakushauriana na viongozi wa *Nadwa,* hivyo kijitabu hiki hakikusomwa katika mkutano ule. Kwa hiyo wajumbe walimhubiri pale mtu mmoja mmoja na walikigawa kijitabu hiki kwa kuwafikishia ujumbe.

SHUKURANI

Kijitabu hicho kilifasiriwa na Sheikh Bakri Abedi Kaluta wa Tanzania. Kisha hapa Makao Makuu katika 'Deski ya Kiswahili' ya Wakalati Tasnif Rabwah, Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani wakaichunguza tafsiri hiyo kwa kuilinganisha na matini ya Kiurdu kwa uangalifu sana na kuidurusu. Aidha ndugu kadha wengine nao wakasaidia kwa njia mbalimbali, kama vile Sheikh Ansar Hussain, Dkt. Muhammad Shafiq Sehgal na Sharifu Tanwir Mujtaba.

Hao wote walioshughulikia kazi hii wanastahili kushukuriwa na kuombewa. Mwenyezi Mungu Awajaalie malipo bora na akubali huduma yao. Aamina

Chaudhry Muhammad Ali, M.A.
Wakilut Tasnif
Tahrik e Jadid,
Rabwah, Pakistan.
20 Desamba, 2014

# التبليغ

يا أهل دار الندوة تعالوا إلى كلمة سواء بيننا وبينكم أن لا تحكّموا إلا القرآن - ولا تقبلوا إلا ما وافق قول
الرحمان - وهذا هو الدين القيّم أيها المتقاعسون - وإن القرآن كتاب خُتم به الهدى - وفيه كتب قيمة وخبر ما يأتي ومضى
فبأيّ حديث بعده تؤمنون - اعلموا أن الخير كله في القرآن وشر الأحاديث ما خالفه فاحذروها أيها المتقون
وكلما خالف هدى القرآن وقصصه فاعلموا أنه سقط ولا يقبله إلا الفاسقون - وإني أنا المسيح وبالحق أمشي وأسيح
ولهذا أنادي وأصيح وأذكّركم أيام الله فهل أنتم تتذكرون - وإني جئتكم ببينة من ربي وعُلّمتُ ما لم تعلموا وأبصرت
ما لا تُبصرون - أتكذبونني ولا تجيئونني ولا تسئلون إن عيسى مات ولا يجيء بإحيائكم فلا تكذّبوا القرآن أيها المجترئون
وإن كان نازلا قبل يوم القيامة كما تزعمون - فلم أنكر لما سئل عن ضلالة النصارى واعتذر بعدم العلم كما أنتم تدرسون
ولم يقل إني أعلم ما أحدثوا بعدي بما رُددتُ إلى الدنيا ورأيتُ ما كانوا يعملون - وكان الحق أن يقول رب إني رجعتُ
إلى الدنيا بإذنك ولبثتُ فيهم إلى أربعين سنة فوجدتهم يعبدونني وأمي وعليه يصرّون فكسرتُ صلبانهم
وأصلحتُ بنيانهم وقتلتُ كثيرا منهم فدخلوا في دين الله وهم يتضرّعون - فاسئلوا عيسى كم لم يكذب يوم القيامة
ويُخفي شهادة كانت عنده كأنه من الذين لا يعلمون * وإني أقسم بالله إني منه فعظّموا حلف الله أتكتمون تتقون -
وإني أُعطيت كثيرا من الآيات وسدّ القرآن طريقا آخر دوني فأين تفرّون - وقد جئتُ على رأس المائة
كما أنتم تعلمون - وخُسف القمر والشمس في رمضان - ليكونا آيتين لي من رب الرحمان - ثم أُنزل الطاعون
لعل الناس يتفكرون - فما لكم لا تنظرون إلى آي الله أو تغاف عيونكم ما تنظرون - أيها الناس عندي شهادة
من الله فهل أنتم تؤمنون - أيها الناس عندي شهادات من الله فهل أنتم تسلمون - وإن تعدّوا شهادات
ربي لا تحصوها فاتقوا الله أيها المستعجلون - أفكلما جاءكم رسول بما لا تهوى أنفسكم ففريقا كذبتم
وفريقا تقتلون أنا نُصرنا من ربنا ولا تُنصرون من الله أيها الخائنون - أقتلتموني بفتاوى القتل ودعاوي
رفعتموها إلى الحكام ثم لا تندمون - كتب الله لأغلبنّ أنا ورسلي ولن تُعجزوا الله أيها المحاربون -
ووالله إني صادق ولست من الذين يختلقون - أتنكرونني وقد تمت عليكم الحجة ألا تردون إلى الله أو أنتم
كمسيحكم خالدون - ألا تتدبرون سورة النور والتحريم والفاتحة أو تكرهون قراءتها
أو على أنفسكم تحرّمون - وهذه رسالة مني أهديتُ لكم يا أهل الندوة
لعلكم تفتحون عيونكم أو تلوح عليكم حجة الله ولا تعتدون بعدها ولا تختصمون -

وإني سمّيتها

## تحفة الندوة

وإني أرسل إليكم رسلي وأنظر كيف يرجعون -
وإني أدعو الله أن يجعلها مباركة لقوم لا يستكبرون - ربّ اشهد أني بلّغتُ ما أمرتَ فاكتبني والذين
يبلّغون رسالاتك ولا يخافون آمين ثم آمين

مطبع ضياء الإسلام قاديان باهتمام حاجي حكيم فضل دين صاحب طبع هوا
تعداد جلد ١٦٠٠

# Tabligh

Enyi watu wa Darun Nadwa! Njooni kwenye neno lililo sawa baina yetu na yenu kwamba tusimfanye yeyote yule kuwa muamuzi isipokuwa Kurani, wala tusikubali chochote isipokuwa kiwe kimeafikiana na kauli ya Rahmani. Na hiyo ndiyo dini iliyo madhubuti enyi wenye kiburi. Na hakika Kurani ni kitabu ambacho kwacho mwongozo umekamilika na ndani yake mna sheria zilizo madhubuti na habari za yale yajayo na yaliyokwisha pita. Hivyo ni hadithi gani kinyume chake mtakazoziamini? Jueni kwamba heri zote zimo ndani ya Kurani; na hadithi mbovu sana ni zile zinazopingana nayo, hivyo mjihadhari nazo enyi wacha-Mungu. Na kila kilichohitilafiana na mwongozo wa Kurani na visa vyake, basi fahamuni kwa hakika hiyo ndiyo takataka na hakuna wanayokubali hiyo ila waasi. Na kwa hakika mimi ndimi Masihi, na kwa haki ninatembea na ninasafiri na ninanadi na kupaza sauti kwa ajili ya Mungu, na ninakukumbusheni siku za Mungu, basi je mtatafakari? Na kwa hakika nimekujieni na ishara ya wazi toka kwa Mola wangu na nimefundishwa yale ambayo hamkufundishwa na nimeona yale ambayo hamkuoa. Je mwanikadhibisha na hamji kwangu wala hamwulizi ya kwamba Isa amekufa, na hatahuishwa na

kumhuisha kwenu. Basi, msiikadhibishe Kurani enyi wajasiri. Na kama alikuwa ateremke kabla ya siku ya Kiyama kama mnavyodhani, basi kwa nini alikataa alipoulizwa kuhusiana na upotevu wa Wakristo, na akatoa udhuru wa kutokuwa na elimu kama mnavyosoma, na hakusema, "Mimi nafahamu waliyoyazua baada yangu, kwa kuwa nilirudishwa duniani na nikaona yale waliyokuwa wakiyatenda. Na ilikuwa ni haki aseme, "Ee Mola wangu, kwa hakika mimi nilirejea duniani kwa idhini yako, nami nikaishi kati yao kwa miaka arobaini na nikawakuta wakiniabudu mimi na mama yangu na wakalishikilia sana hilo. Basi, nikavunja misalaba yao na nikaondoa maradhi zao za zamani na nikawaua wengi miongoni mwao basi wakaingia katika dini ya Mwenyezi Mungu wakinyenyekea. Basi mwulizeni Isa wenu, kwa nini atasema uongo siku ya Kiyama na kuuficha ushahidi aliokuwa nao kana kwamba yu miongoni mwa wasiojua. Nami naapa kwa Mungu kwamba mimi natokana naye, basi kipeni taadhima kiapo cha Mungu ikiwa m wamchao Mungu. Na kwa hakika nimepewa ishara nyingi, na Kurani imeifunga njia nyingine isiyokuwa yangu, sasa mtakimbilia wapi? Na mimi nimekuja mwanzoni mwa karne kama mjuavyo, na mwezi na jua vikapatwa ndani ya Ramadhani ili ziwe alama mbili kwa ajili yangu toka kwa Mola wangu Aliye

Mwingi wa Rehema. Halafu Akateremsha tauni ili watu wapate kutafakari. Mmepatwa na nini kiasi ya kwamba hamzitazami aya za Mungu, au macho yenu yameharibika kwamba hamwoni.

Enyi watu! Mimi ninazo shuhuda toka kwa Allah, je mtaamini? Enyi watu, ninazo shuhuda toka kwa Allah, je mtazikubali? Na kama mkizihesabu shuhuda za Mola wangu, basi hamtaweza kuzihesabu basi Mchani Mungu, enyi wenye papara. Je kila alipokujieni Mtume kwa yale zisiyoyapenda nafsi zenu, basi kundi moja mlilikadhibisha na kundi jingine mnaliua. Kwa hakika tumepewa msaada toka kwa Mola wetu na nyinyi hampati msaada toka kwa Mungu enyi Mahaini. Je mliweza kuniua kwa fatuwa za mauaji au kwa madai mliyoyapeleka kwa mahakimu? Hata hivyo hamwoni haya! Mungu Amekwishaandika kwamba lazima Nitashinda Mimi na Mitume Wangu. Na kamwe hamuwezi kumshinda Mungu enyi mpiganao. Na Wallahi mimi ni mkweli na si miongoni mwa wale wenye hitilafu. Je mwanikataa ilhali hoja zimetimia juu yenu? Je hamtarejeshwa kwa Mwenyezi Mungu au kama Masihi wenu mtaishi milele? Je hamzitafakari sura An Nuur na At Tahriim na Al Fatiha, au mwachukia kuzisoma au mnaziharamisha hizo juu ya nafsi zenu. Na hii ni risala kutoka kwangu ninayowaleteeni kama zawadi, enyi watu wa Nadwa, huenda mkafunua macho yenu au ikatimia

juu yenu hoja ya Mungu, na msipate kutoa udhuru baada yake wala kugombana. Nami nimeiita:

**Tuhfatun Nadwa**

(Zawadi Kwa Nadwa)

Na ninawatumia wajumbe wangu kwenu na nitaona kwamba watarudi na jibu gani.

Nami namwomba Mungu Afanye iwe yenye baraka kwa watu wasio na kiburi. Ee Mola wangu, Shuhudia kuwa nimefikisha yale Uliyoamuru, basi Uniandike kati ya wale wanaofikisha ujumbe wako wala hawahofu. Aamin thumma Aamin.

Kilichapwa katika kivanda cha Ziaul Islam huko
Qadian chini ya usimamizi wa Bwana Haji
Hakim Fazaldin.

## Shairi la Mir Nasir Nawab wa Delhi

*Safina ya Nuhu na Mwito wa Imani ni kitabu cha ajabu chenye shani ya juu.*

*Dini inaboreka kwa kukisoma, kwayo imani inaongezeka.*

*Hiki ni bora kuliko maji ya uhai, kinahuisha roho zilizokufa.*

*Kukisifu barabara sina uwezo, ulimi wangu washindwa kutoa sifa yake.*

*Kitabu hiki chawaongoza wapotevu, ndicho njia ya kuwapatia mwongozo.*

*Hicho ndicho tegemeo la wanyonge, ndani yake mna tiba kwa wasioponeka.*

*Yaliyomo humo hayana kifani, ndicho ishara ya Mjumbe wa Mungu.*

*Siri za dini zinafunguka kwacho, mtu akikisoma kwa makini.*

*Elemu huja na ujahili hutoka, wasiwasi na dhana zaondoka kwacho.*

*Hicho sicho bustani ya dunia bali ni Pepo wanamotembea mahurulaini (wake zao wema) na wavulana (vijana wao wema).*

*Humo mna mito ya maziwa na asali, zimo humo kasri za fahari kila pahali.*

*Safina hii isiyo kifani ndiyo bure, hakuna hapa atakaye ujira.*

*Yule aliyetujalia safina hii, twajitolea kwake nahodha huyo.*

*Ee Mungu, Utujaalie uwezo, kwani U Mwingi wa Rehema na Mwingi wa Ukarimu.*

*Matamanio ya nafsi yatuondoke, shetani atukimbie moja kwa moja.*

*Tuzifuate amri zako usiku na mchana, tukubali amri zako kwa moyo.*

*Uturidhie, nasi tukuridhie pindi itakapotoka roho mwilini mwetu.*

*Nasiri mnyonge ndiye mtumishi wako, yuataka amani yako toka kwako.*

*Ataka rehema yako kutoka kwako, ajitafutia fadhili yako toka kwako.*

*Ee Mola, mwondolee mizigo yake, mrahisishie njia ikufikiayo.*

*Mwingize katika wacha Mungu, Umrehemu, Umrehemu, Ewe Mtukufu.*

*Umsitirie aibu zake Ee Msitiri, kwani anayo dhana njema kwako.*

*Kwa ajili ya Muhammad na Ahmad mwondolee haraka maumivu yake.*

*Yu mtumishi wa imamu kwa moyo wake,*
*msaidie kwa kidhahiri na kisiri.*

Kijitabu kiitwacho

# Zawadi kwa Nadwa

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ[1]

نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ[2]

بہر دم مددے از خدا ہمی آید

کجاست اہل بصیرت کہ چشم بکشاید[3]

Leo tarehe 2 Oktoba 1902 nimepokea kipeperushi kimoja kilichochapwa na Bw. Hafidh Muhammad Yusuf, mstafu, ambamo anaandika kwamba wakati fulani yeye alikiri kwa kutamka kwamba wale watu waliojidai kuwa manabii au wajumbe au mitume kutoka kwa Mungu, watu hao, juu ya uzushi wao ambao makusudio yake yalikuwa ni kuwapoteza watu, waliishi miaka ishirini na mitatu (ambao ndio muda kamili wa siku za utume wa

[1] Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu.

[2] Tunamhamidia na tunamsalia.

[3] Msaada wa Mungu unanifikia kila saa, wenye busara wako wapi ili macho yao yafungue.

Mtume[saw]) bali hata zaidi ya hapo. Na tena ndani ya kipeperushi hicho hicho Bw. Hafidh ameandika kwamba katika kuisaidia kauli yake hii, rafiki yake mmoja aitwaye Abu Ishaq Muhammad Din pia aliandika kijitabu kiitwacho *Qat'ul watiin* ambamo mmeandikwa majina ya wadai waongo pamoja na muda wa madai yao kwa kutaja vitabu vya historia. Muradi kwa jumla wa madhumuni hayo yote waonekana kuwa ni kwamba Bwana Hafidh haiamini aya ya Kurani لو تقوّل[4] wala hataki kuiamini. Wala hana itikadi juu ya aya:

وَاِنۡ یَّكُ كَاذِبًا فَعَلَيۡهِ كَذِبُهٗ[5]

wala hataki kuwa na itikadi hiyo; bali kijitabu cha *Qat'ul watiin* kimeshazikataa aya hizo za Kurani Tukufu, kana kwamba, sawa na rai yake aya zote hizi zimetanguliwa wala haziwajibiki tena kutekelezwa:

وَقَدۡ خَابَ مَنِ افۡتَرٰى[6]

na kama vile aya:

---

[4] Na kama angelizua juu yetu baadhi ya maneno, bila shaka Tungalimshika kwa mkono wa kuume, kisha kwa hakika Tungalimkata mshipa mkubwa [wa moyo]. Na hakuna ye yote katika nyinyi angeweza kumkinga tusimfikie. *Al-Haaqqa*, 69:45-48

[5] Naye akiwa mwongo basi uwongo wake ni juu yake. *Al-Mu'min*, 40:29

[6] Na amekwisha shindwa azushaye uwongo. *Twaa Haa*, 20:62

إِنَّ الَّذِيْنَ يَفْتَرُوْنَ عَلَى اللهِ الْكَذِبَ لَا يُفْلِحُوْنَ[7]

Au kama vile aya:

فَبَدَّلَ الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا قَوْلًا غَيْرَ الَّذِىْ قِيْلَ لَهُمْ
فَاَنْزَلْنَا عَلَى الَّذِيْنَ ظَلَمُوْا رِجْزًا مِّنَ السَّمَآءِ[8]

Zote zimefutwa ambazo kwa sasa haziwajibiki kutekelezwa. Na halafu miongoni mwa aya hizo kuna aya hii pia ambamo Mwenyezi Mungu Anasema kama Nabii huyu angezua baadhi ya mambo kwa kuninasibisha basi Mimi Ningemkamata na kuukata mshipa wake wa uhai. Kana kwamba aya zote hizi zimekataliwa na kijitabu cha *Qat'ul watiin*. Na hii pia yathibitika kutokana na hiyo kwamba maonyo yote haya ya Mwenyezi Mungu yaliyomo ndani ya aya zote hizo hapo juu kuhusiana na wale wazushi yalikuwa ni mambo yaliyokuwa kinyume kabisa na hali ilivyo. Na hawa manabii, amani iwe juu yao, kama wangekuwa wazushi, Mungu Apishe mbali, hata hivyo, kwa kauli ya Bwana Hafidh, wasingeangamizwa, kana kwamba ndani ya serikali ya Mungu hakuna mpango wowote kwa ajili ya wazushi na huko kila udanganyifu

---

[7] Hakika wale wamzuliao uwongo Mwenyezi Mungu hawatafaulu. *Al-Nahl*, 16:117

[8] Lakini waliodhulumu wakabadili kauli ghairi ya ile waliyoambiwa, kwa hiyo tukaiteremsha adhabu juu ya wale waliodhulumu kutoka mbinguni kwa sababu walikuwa wakiasi. *Al-Baqara*, 2:60

unafaulu unaendа tu.[9] Na uwezekano huu unabakia kwamba hata kama awepo nabii amzulie Mungu uwongo basi kusingekuwa na adhabu yoyote kwa ajili yake katika maisha ya duniani, kana kwamba kanuni za serikali ya mwanadamu ndiyo afadhali kuliko kanuni ya serikali ya Mungu, kwani humo (ndani ya kanuni za mwanadamu) matapeli wanakamatwa papo hapo na kupata adhabu. Hapa suala hili pia limetatuliwa kwamba Mtume[saw], hadi Kurani ilipokamilika, ambao ulikuwa ni muda wa miaka ishirini na mitatu, kupata muhula na kuhifadhika na juhudi za wapinzani zilizokuwa ni kwa ajili ya kumuua na baada ya kupata umri kamili kwenda kwa hukumu ya

[9] Wakati kwa rai ya Bwana Hafidh mitume wa uongo pia wanaweza kupata msaada kiasi hiki kwamba juu ya juhudi kubwa za maadui wanaweza wakaishi hadi kuiimarisha dini yao ardhini, hapo kwa msingi huu manabii wote wa kweli watakuwa wameangamia na kutakuwa na tafrani kubwa ndani ya ukweli na uwongo. Na ni dhahiri kwamba kinyume cha mamia ya nia mbaya za maelfu ya maadui na wazushi, na juhudi za wapinzani, kumuweka hai mtume fulani na kuiimarisha dini duniani, huo ni muujiza mkubwa wa Mwenyezi Mungu ambao huwa wanapewa manabii wa kweli na waliokamilika. Hivyo, wakati mitume wa uongo pia washiriki katika muujiza huu, basi kwa sura hii muujiza huu unakuwa sio wa kutegemewa na kunakuwa hakubaki alama yoyote ya wazi kabisa ya ukweli wa nabii mkweli. Lo! Bwana Hafidh, umeumaliza kabisa Uislamu. Ma-hafidh wapaswa kuwa hivyo!!? Mwandishi

Mwenyezi Mungu — kama vile ilivyo pia kwa ajili yangu kuna bishara ya miaka themanini ya kuishi hadi hapo nitakapokuwa nimetimiza kila kitu — mambo haya kwa mtazamo wa Bwana Hafidh siyo muujiza, wala kutimia bishara za aina hii hakutamfanya mtu yeyote afahamike kuwa ni mkweli. Ilmuradi, mimi na vile vile Mtume[saw] sawa na dini ya Bwana Hafidh, hatuwezi kuichukua hifadhi hii na ulinzi wa Mungu kuwa ni dalili ya ukweli wetu, bali hata mwongo pia aweza kushiriki humo. Lakini kwa namna hii basi kauli yote ya Kurani itakuwa ni yenye makosa, kwa sababu yathibitika toka ndani ya Kurani Tukufu kwamba kila mzushi atakamatwa, atadhalilika, ataangamia na hatapata mafanikio.

Na hata akili ya mwanadamu inakubali kwamba mwongo ambaye kwa makusudi anataka kuiangamiza silsila ya Mungu, anapaswa kuangamia. Na maelezo haya haya yanapatikana sehemu mbali mbali ndani ya vitabu vya zamani vya Mungu. Lakini kauli ya Bwana Hafidh ni hii kwamba wengi walitoa madai ya wahyi muongo na ya Unabii mwongo, na waliendelea kutoa madai hayo kwa miaka thelathini na wakaendelea kusisitiza juu ya unabii wao na hadi mwisho hawakuacha kuendelea kutoa madai ya Wahyi wa uongo hadi wakafa wakiwa na hiyo hiyo kufuru, na Mungu Akatia baraka ndani ya umri wao na kazi yao, na Hakuwapa adhabu yoyote. Wala haikuweza

kuthibitika kuwa wakati wowote waliwahi kutubu, wala toba yao haikuwahi kuchapishwa nchini na kuwapasha watu habari juu ya kurudia kwao kuwa Waislamu. Na Bwana Hafidh anasema kwamba uthibitisho wa mambo hayo umeandikwa vizuri sana ndani ya kijitabu cha *'Qat'ul watiin'*. Tena Bwana Hafidh anaandika: 'Mimi sitaki kuchukua zawadi ya rupia mia tano, badala yake ninataka kwamba kwenye mkutano wa mwaka wa *Nadwatul Ulamaa* ambao utaanza mnamo tarehe 9 Oktoba 1902 huko Amritsar ambamo Maskeikh mashuhri wa India watashiriki, Bwana Mirza, yaani mimi, akiri kwa maandishi kwamba mifano ile iliyotolewa (yaani ndani ya kijitabu cha *Qat'ul watiin*) ithibitike kuwa sawa kwa rai ya mwamuzi aliyeteuliwa, yaani kwa rai ya wanazuoni wa Nadwa, yaani wanazuoni wa Nadwa wakubali kwamba ule umri nilioupata kuanzia mwanzoni mwa kupokea kwangu Wahyi, na kwa ule uwazi na kwa zile nguvu zote na kwa ile yakini niliyodai Wahyi wa Mungu na kama vile mimi nimeandika kwa maelfu ya maneno ya Wahyi wa Mwenyezi Mungu kunihusu mimi na kuyatangaza duniani kote, hali kadhalika watu hao nao waliyatangaza na kumzulia Mungu uwongo hata hivyo hawakuangamia bali nao pia wakapata Jumuiya kama yangu, basi hapo yanipasa nifanye toba katika mkutano huo. Mimi nakubali kwamba kama Mungu Amewapa wanazuoni wa Nadwa busara na wanao ucha Mungu na

pia uadilifu na kama wanao wakati wa kutafakari kikamilifu, basi bila shaka wanaweza kutoa fatuwa ya kweli baada ya kuyaona maelezo yangu na ya Qat'ul Watiin ya Bwana Hafidh. Lakini mimi siwezi kuja kwa watu wa Nadwa huko Amritsar kwa sababu sina dhana nzuri na watu hao. Jambo la kweli ni hili kwamba mimi siwafahamu watu hao kuwa ni wacha Mungu (kama siku zijazo Mungu Amfanye yeyote kuwa mcha Mungu basi hiyo itakuwa ni fadhili Yake) wala siwadhani kuwa ni wenye maarifa ya kweli zilizomo ndani ya Kurani, kwa sababu jambo hili limejikita kwenye:

لَّا يَمَسُّهُۥٓ إِلَّا ٱلْمُطَهَّرُونَ[10]

Halafu, ni sababu ipi inifanye mimi niwakubali wao kuwa waamuzi? Naam, kama Masheikh wachache waliochaguliwa miongoni mwao waje Qadian kwa ajili ya kutafuta ukweli, basi mimi naweza kuwahubiria kwa mdomo, waila kazi ya Mungu inaendelea, hakuna mpinzani yeyote awezaye kuizuia. Kuna maana gani kuchukua fatuwa toka kwa mpinzani? Naam, tunachukua fursa ya kuhubiri watu wa Nadwa kutokana na kipeperushi cha Bwana Hafidh. Bwana Hafidh akumbuke kwamba zile hekaya zisizo na kichwa wala

[10] Hapana atakayeigusa [Kurani] ila waliotakaswa. *Al-Waaqi'a*, 56:80

miguu alizoandika ndani ya kijitabu cha *Qat'ul Watiin* kuhusiana na wadai wa uwongo wa unabii, hazitakubalika hata kidogo kama isipothibitika kwamba watu wale wazushi waliendelea kuyasisitiza madai yao na hawakutubu. Na msisitizo (wao) huu wawezaje kuthibitika kama jambo hili lisithibitike kwa njia ya maandishi ya wakati ule ule kwamba watu hao walikufa wakiwa na madai yao hayo hayo ya uwongo na uzushi ya unabii, na hakukuwa na Sheikh yeyote wa zama hizo aliyesalisha sala yao ya jeneza wala hawakuzikwa kwenye makaburi ya Waislamu. Na halikadhalika hekaya hizi haziwezi kamwe kuthibitika kama isipothibitika kwamba uzushi wao wote walioufanya katika umri wao ambao kwa njia ya kumzushia Mungu waliusema kuwa ni maneno ya Mungu huo sasa uko wapi na ni nani na nani wenye kitabu hicho chenye huo Wahyi ili kitabu hicho kitazamwe kwamba je waliwahi kutoa dai lolote la yakini kabisa la Wahyi? Na kwa msingi huu wenyewe waliwahi kudai kwa njia ya kivuli au ya asili kuwa wao ni manabii wa Allah, na wahyi wao waliuchukua kuwa sawa sawa na wahyi wa manabii wengine a.s. kuwa ulitoka kwa Mwenyezi Mungu ili maana ya *Taqawwala* ije kusadikika juu yake. Bwana Hafidh hafahamu kwamba hukumu ya *Taqawwala* inahusika na yakini. Hivyo, kama nilivyoeleza mara kwa mara kwamba maneno haya ninayoyasikilizisha

ni maneno ya Mungu kwa yakini kabisa kama vile Kurani na Taurati zilivyo maneno ya Mungu. Na mimi ni nabii wa Mungu kwa njia ya kivuli na Buruzi na kila Mwislamu anawajibika kunitii katika mambo ya dini na ni wajibu kuniamini kuwa Masihi Mau'udi. Na kila yule ambaye mahubiri yangu yamemfikia, hata kama Yu Mwislamu, ambaye hajanikubali mimi kuwa Mwamuzi wake wala haniamini mimi kuwa ndiye Masihi Mau'udi wala haukubali Wahyi wangu kuwa ni ule uliotoka kwa Mungu, mtu huyo atakamatwa huko mbinguni, kwa sababu jambo alilostahili kulikubali katika wakati wake alilikataa. Mimi sisemi hivi tu kwamba kama ningekuwa mwongo ningeangamizwa, bali nasema pia kwamba mimi ni mkweli kama walivyokuwa akina Musa, Isa, Daudi na Mtume Mtukufu[saw], na Mungu Ameonyesha zaidi ya ishara elfu kumi kwa ajili ya kunisadikisha. Kurani imenitolea ushahidi, Mtume[saw] amenitolea ushahidi, Manabii wa zamani wameainisha zama za kuja kwangu ambazo ndio zama hizi hizi, na Kurani pia yaainisha zama za ujaji wangu ambazo ndio hizi hizi. Na mbingu pia imenitolea ushahidi na ardhi pia, na hakuna nabii yeyote yule ambaye hajatoa ushahidi kwa ajili yangu. Na haya ambayo nimesema kwamba ninazo ishara elfu kumi, hayo nimeandika kwa kutosheleza, waila ninaapa kwa Dhati Yule ambaye uhai wangu u mkononi mwake kwamba

kama kuwepo na kitabu cheupe (yaani daftari) chenye juzu[11] hata elfu moja na humo nitake kuandika dalili za ukweli wangu, basi mimi nina yakini kwamba kitabu hicho kitamalizika na dalili hizo hazitamalizika. Mwenyezi Mungu Anasema ndani ya Kurani Tukufu:

وَإِن يَكُ كَاذِبًا فَعَلَيْهِ كَذِبُهُ ۖ وَإِن يَكُ صَادِقًا يُصِبْكُم
بَعْضُ الَّذِي يَعِدُكُمْ ۖ إِنَّ اللَّهَ لَا يَهْدِي مَنْ هُوَ مُسْرِفٌ كَذَّابٌ ﴿٢٩﴾[12]

Yaani kama yu mwongo, basi ataangamia mbele ya macho yenu na uongo wake utamwangamiza mwenyewe; lakini kama yu mkweli, basi hapo baadhi yenu watalengwa na matabiri yake na wataiondoka dunia hii mbele ya macho yake. Sasa mnijaribu kwa kipimo hiki kilichomo ndani ya maneno ya Mungu na myapime madai yangu. Je hii si kweli kwamba Masheikh hao hawakuiachia fursa hata kidogo ya kuniangamiza? Kwa kutayarishia fatuwa za kunikufurisha miguu yao imechakaa kwa kwenda huko na kuko; kwa kuchapisha vipeperushi vya matusi waliwashinda hata Mashia; kesi za mauaji zikatengenezwa dhidi yangu na mara nyingi nikafikishwa hadi mahakamani kwa kutuhumiwa na tuhuma za jinai. Wale wanijiao wakafanyiwa yale mateso ambayo mfano wa

[11] Hapa neno 'juzu' ni istilahi ya uchapaji, maana yake kurasa 16. Basi Juzu 1000 ndiyo kurasa 16,000. Mwenezi.

[12] *Al-Mu'min*, 40:29

kashfa zake, udhalilishwaji wake na udhia wake haupatikani duniani kote isipokuwa katika maisha ya Masahaba walipokuwa Makka. Baadhi ya wale waliohusiana nami waishio nchi za nje waliuawa katika nchi hizo hizo. Ilmuradi, hakuna yeyote awezaye kukataa kwamba zilitumika juhudi zote kwa ajili ya kunifanya nitoweke na kuwazuia watu wasinijie na haikuachwa juhudi yoyote. Hata shughuli nyingi zisizokuwa na haya zilidhihirika kutoka kwa baadhi ya Masheikh hao hao. Taarifa za uongo dhidi yangu zilipelekwa na bila sababu yoyote serikali ikachochewa dhidi yangu kwa mambo yasiyo sahihi. Lakini je mnajua matokeo yake mwishoni yalikuwaje? Yalikuwa hivi kwamba mimi nikazidi kupata maendeleo. Watu hawa waliposimama kunikufurisha na kunikadhibisha na kutoa utabiri kwamba kwa haraka mno tutamuangamiza mtu huyu, wakati huo mimi sikuwa na Jumuiya kubwa, bali walikuwepo watu wachache tu walioweza kuhesabika kwa vidole, bali katika zama za Barahiine Ahmadiyya, wakati Barahiine Ahmadiyya kilipokuwa kikichapwa mimi nilikuwa peke yangu. Nani awezaye kuthibitisha kwamba wakati huo nilikuwa na hata mtu mmoja pamoja nami. Hizo zilikuwa ni zama zile ambapo Mwenyezi Mungu Alinipasha habari ndani ya bishara zaidi ya hamsini kwamba: ‘Ingawa wakati huu wewe uko peke yako lakini unakuja ule wakati

ambapo halaiki ya watu watakuwa pamoja nawe, na halafu unakuja ule wakati ambapo utapata adhama kiasi hiki kwamba wafalme watatafuta baraka toka katika nguo zako, kwa sababu wewe utapewa baraka. Mungu Yu Mtakatifu, Hufanya Apendacho. Ataieneza ardhini silsila yako na Jumuiya yako na Atawapa baraka na kuwaongeza (kwa idadi) na Ataistawisha heshima yao ardhini maadamu watashikamana na ahadi Yake. Sasa tazameni kwamba hizo bishara za Barahiine Ahmadiyya ambazo tafsiri yake imeandikwa, ilikuwa ni katika zama ambapo hakukuwa na yeyote pamoja nami duniani wakati Mungu Aliponifundisha dua hii:

رَبِّ لَا تَذَرۡنِیۡ فَرۡدًا وَّ اَنۡتَ خَیۡرُ الۡوٰرِثِیۡنَ[13]

Yaani, Ee Mungu, Usiniache peke yangu, na Wewe Ndiwe Mrithi bora kabisa. Hii dua iliyofunuliwa imeandikwa ndani ya Barahiin. Ilmuradi, kwa ajili ya wakati huo Barahiine Ahmadiyya chenyewe kinatoa ushahidi kwamba mimi kwa wakati huo nilikuwa ni mtu nisiyejulikana, lakini leo, juu ya juhudi za kunipinga, wapo ndani ya Jumuiya yangu watu zaidi ya laki moja katika sehemu mbali mbali. Je huu ni muujiza au sio kwamba imetumika kila aina ya njama katika kunipinga na kuniangusha, mipango ikafanywa, lakini Masheikh

[13] Al-Anbiyaa, 21:90

wote hawa na marafiki zao, wadogo kwa wakubwa, wote wakashindwa. Kama huu sio muujiza basi (Masheikh) wa Nadwa waliovaa makanzu makubwa wenyewe waeleze kwamba muujiza ni jina la kitu gani. Kama mimi sio mtu wa miujiza basi mimi ni mwongo. Kama kifo cha Bin Mariam hakithibitiki ndani ya Kurani basi mimi ni mwongo. Ikiwa hadithi ya Mi'raji haikumketisha Isa baina ya roho za wafu basi mimi ni mwongo. Ikiwa Kurani ndani ya Sura Nuur haikusema kuwa Makhalifa wa umati huu watatokana na umati huu huu basi mimi ni mwongo. Kama Kurani haikuniita jina Bin Mariam basi mimi ni mwongo. Enyi wanadamu mfao! Zindukeni na mfikiri kwamba mbali na hayo muujiza unakuwa ni kitu gani kwamba baada ya mapambano ya kiasi hiki na wapinzani hatimaye bishara zile za Barahiine Ahmadiyya zimetokea kuwa za kweli zilizotolewa miaka ishirini na miwili kabla ya leo. Nyinyi hamuwezi kuthibitisha kwamba katika zama hizo kulikuwa na hata mtu mmoja pamoja nami, lakini kwa wakati huu kama watu wa Jumuiya yangu wafanywe kuishi sehemu moja, basi nina yakini kwamba mji ule utazidi hata mji wa Amritsar, ilhali katika zama zile za Barahiin wakati bishara hii ilipotolewa mimi nilikuwa peke yangu tu. Halafu kama kusingekuwa na zahama ya masheikh, bishara ya Barahiine Ahmadiyyah isingepata shani maradufu, lakini sasa

juhudi za upinzani za Masheikh na wafuasi wao zimeutukuza maradufu muujiza huu. Na badala ya kwamba, sawa na madhumuni ya:

وَاِنْ يَّكُ كَاذِبًا فَعَلَيْهِ كَذِبُهٗ[14]

siyo tu nimeondolewa lawama na alama iliyotajwa katika aya hii kwa sababu ya kuwa kwangu mkweli, bali sasa mbali na hilo, bishara zenye shani za Barahiine Ahmadiyyah zilizokwisha enezwa duniani miaka ishirini au ishirini na miwili kabla ya leo tayari zimeshatimia na maelfu ya watu na wataalamu waliokamilika wameungana nami. Sasa itazameni sehemu ya pili ya aya hii:

وَاِنْ يَّكُ صَادِقًا يُّصِبْكُمْ بَعْضُ الَّذِىْ يَعِدُكُمْ[15]

Kipimo hiki pia kimetimia kwa njia ya kimuujiza namna gani. Mwenyezi Mungu Amesema kwa kuniambia:

انّی مهین من اراد اهانتک

kila mtu atakayekudhalilisha basi huyo hatakufa hadi aone kudhalilika kwake. Sasa waulizeni hao Masheikh kwamba je katika kukabiliana nami waliiona dhila yoyote kwa amri ya Mwenyezi Mungu au la? Sasa ni nani mwenye kunikashifu awezaye kusema kwamba bishara hii ya Kurani ambayo ni:

---

[14] *Al-Mu'min*, 40:29

[15] *Al-Mu'min*, 40:29

يُّصِبۡكُمۡ بَعۡضُ الَّذِىۡ يَعِدُكُمۡ [16]

Haikutimia kwa ajili ya kunisaidia, bali Kurani Tukufu imeelezea kwa neno la BAADHI kwamba kwa kutimia bishara ya adhabu mfano wa BAADHI unatosha, na sehemu hii mifano si michache. Je humu mna dhila ndogo kwa wapinzani kwamba Ghulam Dastgir ndani ya kitabu chake cha 'Fat-he Rahmani' yaani ndani ya ukurasa wa 27 baada ya kuniombea dua mbaya kwa maneno ya kawaida, yaani baada ya kuomba dua mbaya dhidi ya mwongo miongoni mwa pande (zetu) mbili, yeye mwenyewe akafa baada ya siku chache tu:[17] Muhammad Hasan wa Bhiin aliandika dhidi yangu, kwenye maandiko yake 'Laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya waongo', hakuweza kukimaliza hicho kitabu na akafa kwa adhabu kali sana. Pir Mehr Ali Shah aliandika dhidi yangu ndani ya kitabu chake 'Laana ya Mwenyezi Mungu iwe juu ya waongo', yeye mara tu akakamatwa katika kosa la wizi

[16] *Al-Mu'min*, 40:29

[17] Tazameni, je huu sio muujiza kwamba yule Sheikh aliyewaandikisha baadhi ya Masheikh wasiojua kitu wa huko Makka fatuwa ya kunikufurisha akafa mwenyewe alipofanya Mubahala. Mwandishi

kwa njia hii kwamba[18] kumbe kitabu chake chote aliibia kwa mfile Muhammad Hasan na kujidai kwamba yeye ndiye aliyekiandika na akasema uongo na akakipa jina la 'Saife Chishtiai'. Halafu msiba wa tatu ni huu kwamba hoja zote za upinzani alizotoa mfile Muhammad Hasan dhidi ya kitabu changu cha I'jaazul Masih, hoja zote hizo zikathibitika kuwa batili. Akafa kabla hata ya kukipitia tena kitabu chake. Mjinga huyu asiye na ufahamu wa Kiarabu akazifahamu hoja zote hizo (za kunipinga) kuwa ni sahihi. Sasa hebu semeni, hii pia ni aina ya mauti au siyo kwamba ameiba mswada wa kitabu, na wizi huo ukajulikana na halafu akiwa kiongozi kasema uongo wa

[18] Mehr Ali, kwa kutegemea kukosoa kwa mfile Muhammad Hasan, akatoa shutuma hii ya kijahili juu yangu kwamba mimi nilinakili baadhi ya mifano mashuhuri ya Kiarabu na baadhi ya misemo iliyonukuliwa pia na Maqaamaat Hariri n.k.' hizo zapatikana ndani ya kitabu changu kama nukulu ambazo hazizidi mistari miwili mitatu. Kana kwamba, kwa mtazamo wa mjinga huyu, huu ndio wizi. Kwa hiyo, wakati huo ilikuwa ni lazima kwamba bishara hiyo itimie wazi wazi kwamba:انّی مهین من اراد اهانتک (yaani nitamdhalilisha kila atakayedhamiria kukudhalilisha), hivyo yeye akathibitika kuwa mwizi wa kitabu kimoja kizima na akasema uongo na akazifuata hoja zenye shutuma zisizokuwa sahihi na hakuweza kutanabahi kama hayo ni makosa. Kwa namna hii akawa amekamatwa kwenye makosa matatu makubwa. Je huu sio muujiza? Mwandishi.

wazi kabisa kwamba yeye ndiye aliyekiandika, na halafu hicho alichokiiba kilikuwa na makosa kiasi hiki kana kwamba kilikuwa ni najisi. Je, adhabu ya Jahannam ni zaidi ya adhabu hii?[19] Muhtasari wa maneno kwa Bwana Hafidh ni huu kwamba kufanya kwangu toba haitatosha tu kwamba kama kimuhali kitoke kitabu cha mwenye kudai unabii anachochukulia kuwa wahyi wa Mungu kama vile Kurani Tukufu, (kama yalivyo madai yangu) ambacho kuhusu hicho aseme kuwa hamna shaka ndani yake, kama nisemavyo mimi, halafu ithibitike pia kwamba yeye alikufa bila ya kufanya toba na kwamba Waislamu hawakumzika ndani ya makaburi yao na hakuhiliki kwa adhabu yoyote ile, hata hivyo huyo mdai wa unabii wa uwongo hawezi kulingana nami kwa sababu ipo miujiza pia inayonisaidia. Na juu ya yote hayo mimi nina yakini kwamba kama Bwana Hafidh aendelee kujaribu hadi

[19] Wizi huu wa Mehr Ali na halafu kuyategemea makosa kwa ujahili, na kwa ujinga kumsema kuwa Mwana wa Mariam yu hai na mambo mengineyo ambayo yamemkuta moja kwa moja kutokana na ujahili na ujinga, kuhusiana na hayo kuna kitabu cha muhimu sana ninachokiandika kinachoitwa Nuzuulul Masih ambacho kitavunja tari ya Kichishti na itabakia vumbi tu ndani yake itakazoingia ndani ya macho ya Mehr Ali na kuyafanya maisha yake kuwa machungu. Kitabu hiki kimeshachapwa hadi vifungu 11 (yaani kurasa 176). Mwandishi

aiage dunia au aandikishe pia kwa Abu Ishaq Muhammad Din mwingine nakala elfu moja za *Qat'ul Watiin* nyingine na hata kama mtu wa aina hiyo atamani kujiua na akate mshipa wake mkubwa lakini hata hivyo Bwana Hafidh hataipata bahati kwamba kama vile mimi, kwa takriban miaka thelathini na mitatu nimekuwa nikitangaza wahyi wangu kwa mfululizo, kwa namna hii hii aweze kutoa mjumuisho wa wahyi wake wa miaka ishirini na mitatu mfululizo ambao kwao, kama vile mimi, aliubainisha kwa kula kiapo kwamba wahyi huu kwa yakini kabisa ni maneno ya Mwenyezi Mungu, kama nimesema uongo basi laana ya Mungu iwe juu yangu kama vile mimi nilivyokwisha andika ndani ya vitabu vyangu kwa maneno haya haya. Hili ni jambo la ngazi ya chini tu kwamba nipimwe pamoja na waongo, lakini mimi zaidi ya hiyo ninao uthibitisho wa ukweli wangu kwamba maelfu ya miujiza yameshadhihiri hadi sasa yenye maelfu ya mashahidi, na Kurani Tukufu inanisadikisha. Je hii sio haki yangu kwamba wakati wa kupambanua huku niwaombeni thibitisho hizo kumhusu mwongo yeyote mnayemtaja? Hebu, elezeni kwamba ni nani minghairi yangu ambaye kwaye, kwa mujibu wa Hadithi ya Dar Qutni, bishara ya kupatwa jua na mwezi ilitimia? Ni kwa ajili ya nani, kwa mujibu wa Hadithi

sahihi, ugonjwa wa tauni uliibuka? Ni kwa ajili ya nani nyota yenye mkia ilitokeza? Ni kwa ajili ya nani ishara za Lekhram n.k. zilidhihiri? Lakini kundi la Nadwatul ulamaa kama linataka liwe sawa sawa na jina lake, basi sasa kwa ajili ya mwongozo wake binafsi, hata kama Bwana Hafidh ajipatie sehemu katika huo au la, hata kiasi hicho pia chaweza kutosha kwamba limuombe Bwana Hafidh uthibitisho kwa kiapo wa hao wadai wa unabii ambao wahyi wao wa uongo ulidumu kwa muda wa miaka ishirini na mitatu kama ule wa Kurani Tukufu, na limuombe uthibitisho kwamba ni wapi walipoeleza kwa kula kiapo kwamba sisi kwa hakika ni manabii na wahyi wetu ni wa yakini kabisa kama ule wa Kurani. Na pia liombe uthibitisho huu kwamba je watu hao walitolewa fatuwa za kukufurishwa na Masheikh wa zama hizo au la? Na kama hawakukufurishwa, sababu yake ni nini? Je Masheikh wa aina hiyo walikuwa mafasiki na waovu au la ambao walidhihirisha hali ya kutojali hivyo katika mambo ya dini. Na pia liombe uthibitisho huu kwamba watu hao walizikwa ndani ya makaburi gani? Je ndani ya makaburi ya Waislamu au penginepo? Na je waliuawa ndani ya dola ya Kiislamu[20] au walipitisha umri wao kwa amani? Bwana

[20] Kwa kutoa uthibitisho wa "ndani ya dola ya Kiislamu" hakutoshi kwamba mtu wa aina hiyo ambaye alikuwa na madai ya unabii

Hafidh aombwe kuleta uthibitisho huu na halafu baadhi ya Masheikh watakaochaguliwa wa Nadwa waje Qadian kwa ajili ya kutaka uthibitisho wa miujiza yangu na dalili zingine kutokana na aya za wazi wazi za Kurani na Hadithi na wapate toka kwangu uthibitisho wa miujiza na dalili yaani wa aya wazi wazi za Kurani na Hadithi. Halafu, kama kulingana na suna ya manabii a.s., sikuweza kutoa uthibitisho kamili, basi mimi niko radhi kwamba vitabu vyangu vichomwe moto. Lakini kufanya juhudi ya aina hii ni kazi ya Mchamungu, Nadwa ina haja gani ya kusumbuka kiasi hiki na wanaijalije Akhera hata wamwogope Mungu. Lakini Masheikh wa Nadwa, kila mmoja wao akumbuke kwamba hawawezi kuishi duniani milele. Vifo vinaita na ule mchezo wanaojishughulisha nao wanaouita ndiyo dini, Mungu anauona mbinguni na Anajua kuwa huo si dini. Wao wanaridhika na ganda na hawana habari ya kiini. Hii si kuitakia mema Islam bali ni kuitakia mabaya. Laiti wangekuwa na macho basi wangefahamu kuwa dhambi kubwa imefanywa duniani

hakuzikwa ndani ya makaburi ya Waislamu wala jeneza lake halikusaliwa. Bali kwa ajili ya uthibitisho wenye kutosha, hii pia itapaswa kuthibitishwa kwamba yeye aliuawa pia kwa sababu yeye alikuwa ni murtad. Lakini kama bwana Hafidh atoe uthibitisho huu, hivyo inakuwa kana kwamba atalikubali jambo lile alilokuwa akilikimbia. Mwandishi.

kwamba Masihi wa Mungu amekataliwa. Jambo hili kila mtu atalifahamu baada ya kufa. Na Bwana Hafidh ananitishia kwamba 'kama hauji Amritsar basi duniani kote utafahamika kuwa ni mwongo katika madai yako.' Ewe bwana Hafidh! Dunia hii ni ya nani? Ni yako au ni ya Mungu? Nyinyi watu hata sasa mwanidhania kuwa mwongo, baada ya hapo nini mtakachonidhania? Dunia yenu hatuijali. Kila nafsi iko chini ya nyayo za Mungu wangu. Sikiliza ewe Hafidh mwenye fikara mbovu! Una habari gani kwamba msaada wa Mungu unaniendeleza kiasi gani. Hata kama hasidi ajifie, maendeleo haya hayawezi kusita kwa sababu yanatokana na mkono wa Mungu na yanaafikiana na ahadi ya Mungu, hayatokani na mkono wa mwanadamu. Mungu Ameijaza miji ya Panjab na India kwa wanajumuiya wangu. Ndani ya miaka michache watu zaidi ya hata laki moja wamefanya baiati yangu. Je bado hujaelewa kwamba ni yupi anayesaidiwa mbinguni? Nadhani watu karibu ya elfu kumi wamejiunga ndani ya Jumuiya yangu kupitia tauni, nami nina yakini kwamba ndani ya siku chache ardhi itajaa jamaat yangu. Ewe bwana Hafidh! Je wewe siye bwana Hafidh yule yule ambaye uliniambia moja kwa moja kwamba Sheikh Abdullah wa Ghazni alikuwa akisema kwamba nuru moja imeteremka Qadian ambayo

watoto wangu wameikosa. Yasikitisha kwamba umemuudhi bwana Abdullah kaburini. Je ilikuwa lazima kwako kutumia njia hii ya upinzani katika kuipinga kauli yake? Halafu, je Mian Muhammad Yaqub sio ndugu yako hasa? Ulipaswa hata kumwuliza yeye. Yeye kwa karibu miaka kumi anapiga kelele kwamba yeye pia aliambiwa na Sheikh Abdullah wa Ghazni kuhusu Qadian kwamba nuru itateremkia humo humo Qadian nayo ndiye Ghulam Ahmad. Na alipasha habari kwamba hadi sasa yeye amesimama katika ushuhuda huu na barua yake ipo. Halafu wewe baada ya kuitwa Hafidh humtegemei Hafidh wa Kweli. Unasema uwongo kwa kuwaogopa watu. Mimi nipo katika kutafakari kwamba hizi zilikuwa ni kashf za aina gani za Bwana Abdullah ambazo zimezikwa pamoja naye. Mtu kama wewe uliye Khalifa wake mkubwa pia hukuzithamini. Amani kwa yule aliyeufuata mwongozo.

Mwandishi:
Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian.
4 Oktoba 1902.

## Bishara kubwa kwa Waislamu wote na kwa ajili ya wote watafutao ukweli

Hadhrat Isa[as] ambaye uhai wake wa kimuujiza na kwenda kwake mbinguni pamoja na mwili wake kinyume na maneno ya Kurani na juu ya kwamba hakuwa mfu hata hivyo amekwisha ingia ndani ya roho za manabii waliokwisha kufa ambao kwa namna fulani wamekwisha ingia peponi, haya yote ni mambo ambayo kwa hakika yalikuwa ni doa kwa ajili ya dini ya kweli. Na pia tangu muda mrefu Waislamu wenye kuamini Mungu mmoja walikuwa na deni ya watu wa magharibi wanoabudu kiumbe, na Waislamu wajinga nao pia baada ya kulikiri deni hili walijiongezea riba ya Wakristo iliyosababisha malaki ya Waislamu katika nchi hii ya India kuritadi na kuangukia ndani ya mikono ya Wakristo wakiwa rehani na haikuonekana njie yoyote ya kulipa deni. Wakristo walipokuwa wakisema mola wetu Yesu Masihi alipanda mbinguni akiwa hai na mwili wake, akaonyesha nguvu kubwa sana, maana alikuwa  Mungu, lakini nabii wenu baada ya kuhama (Makka) hakuweza kufika Madina kwa kuruka. Kwa siku tatu alikaa akijificha ndani ya pango la

Thaur, hatimaye akafika Madina kwa shida sana, hata hivyo hakuishi muda mrefu, akafariki baada ya miaka kumi na sasa yupo kaburini na ndani ya ardhi. Lakini Yesu Masihi yupo hai mbinguni na ataishi milele na ndiye yeye huyo huyo atakayeteremka tena toka mbinguni kuleta uadilifu duniani. Kila yule asiyemfahamu yeye kuwa Mungu atakamatwa na kuingizwa motoni.

Waislamu hawajui jibu lake lolote, walikuwa wakiaibika na kudhalilika sana. Sasa 'uhakika' wa uungu wa Yesu Masihi umedhihirika sana, siri yote ya kupaa mbinguni imefichuka. Kwanza ni kudhihiri zaidi ya vitabu elfu moja vya utibabu vilivyotafsiriwa na Warumi, Wayunani, Wamajusi na Wakristo katika zama za kale na baada ya wote Waislamu pia wakatafsiri ambamo imeandikwa dawa ya Marhamu ya Isa. Na imeelezwa ndani ya vitabu hivyo kwamba marhamu haya yalitengenezwa kwa ajili ya Isa yaani kwa ajili ya majeraha yake ya msalabani. Baada ya hayo kaburi pia la Hadhrat Isa[as] limeibuka huko Kashmir. Halafu baada ya hayo vimeibuka vitabu vya kale vya Kiarabu na Kifarsi ambavyo baadhi yao viliandikwa miaka elfu moja iliyopita na vinatoa ushahidi wa kifo cha Hadhrat Isa[as] na vinataja kaburi lake kuwepo Kashmir. Na halafu baada ya yote ile habari tuliyoipata leo ni habari ambayo kana kwamba imeileta siku ya Idi kwa ajili ya Waislamu nayo ni hii kwamba siku hizi hizi karatasi

fulani iliyosainiwa na mwanafunzi wa Yesu, Petro na kuandikwa katika lugha ya Kiebrania cha kale imevumbuliwa huko Yerusalem ambacho kimejumuishwa ndani ya kitabu cha Safina ya Nuhu. Kutokana na hicho inathibitika kwamba takriban miaka hamsini baada ya tukio la msalaba Hadhrat Isa[as] alifariki hapa hapa duniani na kampuni moja ya Kikristo imeinunua karatasi hiyo kwa thamani ya rupiya laki mbili na nusu, kwa kuwa uamuzi umeshafanyika kuwa hayo ni maandiko ya Petro. Na ni dhahiri kwamba baada ya kujumuika uthibitisho mwingi kiasi hiki ambao ni shuhuda madhubuti kweli kweli, halafu kutoepukana na itikadi hii ya ovyo kwamba Isa yu hai inakuwa ni uchizi tu. Mambo yanayohisika na kuonekana hayawezi kukataliwa. Hivyo enyi Waislamu! Hongereni, leo ni siku ya Idi kwa ajili yenu, ziacheni zile itikadi za uongo za mwanzoni na sasa muifanye itikadi yenu iafikiane na Kurani. Cha kusisitiza ni kwamba ushahidi huu wa mwisho ni ushahidi wa mwanafunzi mkuu wa Hadhrat Isa[as]. Huyu ndiye yule mwanafunzi wa Yesu ambaye katika maandishi yake yaliyopatikana, mwenyewe anatumia maneno haya kwa ajili ya ushahidi huu kwamba: 'Mimi ni mtumishi wa mwana wa Mariamu na ninaandika barua hii nikiwa na umri wa miaka tisini ambapo miaka mitatu imeshapita tangu mwana wa

Mariamu afariki'. Lakini jambo hili lathibitika katika historia na wanazuoni waliobobea wa Kikristo wanalikiri jambo hili kwamba muda wa kuzaliwa wa Petro na wa Hadhrat Isa[as] ulikaribiana na wakati wa tukio la msalaba umri wa Hadhrat Isa[as] ulikuwa takriban miaka thelathini na mitatu na umri wa Hadhrat Petro kwa wakati huo ulikuwa kati ya miaka thelathini hadi arobaini.

(Tazameni kitabu cha Smith's Dictionary, jalada la 3, uk. 2446 na Moti Tulus New Testament History na vitabu vingine vya historia)

Na kuhusiana na barua hiyo wanazuoni wakubwa wa kikristo, baada ya kufanya utafiti mkubwa, walifikia uamuzi huu kwamba hiyo ndiyo sahihi, na wakadhihirisha furaha kubwa kwa ajili hiyo. Na kama vile tulivyokwisha andika, maandiko hayo yalitazamwa kwa heshima na taadhima sana hata kwamba kiasi kikubwa cha fedha walipewa warithi wa mtawa huyo mtukufu kwa ajili yake ambaye barua hiyo ilivumbuliwa toka kwenye maktaba yake baada ya kifo chake. Na kwa rai yetu, juu ya usahihi wa karatasi hiyo kuna dalili nyingine yenye nguvu kwamba karatasi hiyo imetoka kwenye maktaba ya mtu ambaye itikadi yake ilikuwa ni ya kikatoliki, na sio tu kuwa alikuwa akiukiri uungu wa Hadhrat Isa[as] bali alikuwa akiukiri hata uungu wa Hadhrat Mariamu pia.

Yeye alikuwa ameziweka tu karatasi hizo katika nyaraka za kale zenye baraka. Na kwa kuwa kilikuwa ni Kiibrania cha kale na hata mfumo wa uandishi ulikuwa ni wa kale, hivyo yeye alikuwa tu hayaelewi madhumuni yaliyokuwemo. Hii ni ishara kubwa. Mbali na ushahidi huu mpya uliotoka kwenye barua ya Hadhrat Petro, hata miongoni mwa Wakristo wa awali kuna baadhi ya madhehebu yanayokiri jambo hili kwamba Hadhrat Isa[as] alitolewa msalabani katika hali ya kuzimia kulikofanana na kifo na kupata matibabu ndani ya pango fulani kwa siku tatu na kuelekea sehemu nyingine baada ya kupata ahuweni ambapo aliishi kwa muda mrefu. Maelezo ya itikadi hizi yameandikwa kwa kirefu ndani ya vitabu vya Kiingereza miongoni mwao vikiwa ni *'New Life of Jesus'* (maisha mapya ya Yesu) cha *Strauss* na kitabu cha *'Modern Doubt and Christian belief'* na kitabu cha '*Supernatural Religion'* ambapo baadhi ya ibara tumeziingiza ndani ya kitabu chetu cha *Tohfa Golarwiya*.

Mwandishi:
Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian.
6 Oktoba 1902.